TANGAZO LA SERIKALI Na. 83 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 5(1))*

AMRI YA KUPANDISHA HADHI HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI YA MWAKA 2025

KWA KUWA, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa alitoa Notisi ya Kusudio la Kupandisha Hadhi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kama ilivyoainishwa katika Notisi hiyo iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, Tangazo la Serikali Na. 818 la Mwaka 2024;

NA KWA KUWA, baada ya muda wa Notisi kuisha, hakuna pingamizi au wasilisho lolote lililopokelewa na Waziri kuhusu kusudio la kupandisha hadhi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji;

HIVYO SASA, mimi MOHAMED OMARY MCHENGERWA, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, katika utekelezaji wa madaraka niliyopewa na kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, natoa Amri kama ifuatavyo:

Jina

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupandisha Hadhi Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ya Mwaka 2025.

Tamko

**2**. Eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kama lilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza, linatangazwa kuwa Mamlaka ya Halmashauri ya Mji.

Jina la Halmashauri na nembo

**3**. Halmashauri ya Mji iliyotangazwa chini ya Amri hii itajulikana kama Halmashauri ya Mji Rufiji na itakuwa na nembo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

Muundo wa Halmashauri

**4**. Wajumbe wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji watakuwa wajumbe wa Halmashauri ya Mji Rufiji.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MIPAKA YA ENEO LA MAMLAKA YA HALMASHASURI YA MJI RUFIJI

"Kuanzia katika Kituo cha Upimaji VP 706 kwa umbali wa kilomita 11, kisha kugeukia Kaskazini Magharibi kwa kilomita 5.8 hadi Kituo cha Upimaji VP 717, kisha kugeukia Kaskazini Mashariki kupitia umbali wa kilomita 5.1 hadi Kituo cha Upimaji VP 733. Kisha kuelekea Kaskazini kupitia vituo vya upimaji VP 729, VP 727, VP 731 kwa umbali wa kilomita 22, kisha kugeukia Kusini Mashariki kupitia vituo VP 726 na VP 725 kwa kilomita 10.2; kisha mpaka hugeukia Kaskazini kwa kilomita 4.6 kando ya mto mdogo unaoungana na Mto Rufiji mkubwa katika eneo la Msomeni. Kutoka hapo, hugeukia Magharibi na kwenda kando ya Mto Rufiji kwa umbali wa kilomita 23.9 hadi Kituo cha Upimaji VP 747, kisha kugeukia Kaskazini Magharibi kwa umbali wa kilomita 22 kupitia vituo vya upimaji IK4, VP 757, VP 822, kisha kubadilisha mwelekeo kuelekea Magharibi na kupita kupitia vituo vya upimaji VP 816, VP 358 kwa umbali wa kilomita 20.8; kisha mpaka hugeukia Kaskazini Magharibi kupitia vituo vya upimaji VP 317, VP 846, VP 845, VP 840, kisha kugeukia Kaskazini Mashariki kwa kilomita 26.8 hadi Kituo cha Upimaji VP 567 kwenye mpaka wa Wilaya ya Kisarawe na Wilaya ya Kibiti. Kutoka Kituo cha VP 567, hugeukia Magharibi kwa kilomita 35.2 kupitia vituo vya upimaji NP6, NP5, NP4, VP 849, VP 641, VP 583, na VP 852, kisha kuelekea Magharibi kwa kilomita 11.4 hadi GN inayofafanua mipaka ya Wilaya ya Kisarawe, Wilaya ya Morogoro Vijijini, na Wilaya ya Rufiji. Kutoka kwenye mahali panapounganisha wilaya hizo tatu, ambazo ni Wilaya ya Rufiji, Wilaya ya Kisarawe, na Wilaya ya Morogoro Vijijini, kuelekea Magharibi kwa kilomita 50.99 katika Behobeho Upstream, kisha kugeukia Kusini Magharibi kwa umbali wa kilomita 8.4 hadi Kilele cha Hugo. Kisha kubadilisha mwelekeo kuelekea Kusini kwa kilomita 18.8 hadi kufikia Mto Rufiji na Mto Sumbadsi, kisha kuendelea kando ya Mto Rufiji kwa kilomita 16.5 hadi kugusa Mto Ruaha Mkubwa na Mto Rufiji. Kisha kando ya Mto Rufiji kwa umbali wa kilomita 2.8 hadi mahali ambapo Mto Mkumbiso unaungana na Mto Rufiji, kisha kugeukia Kusini Mashariki kwa kilomita 26.8 hadi Mto Lihuni, kisha kugeukia zaidi Kusini Magharibi kwa kilomita 47.6 hadi kijito kinachoelekea kwenye Mto Lukuliro. Kisha kuelekea Kusini Mashariki kwa kilomita 26.17 hadi Kituo cha Upimaji ZAE1, kisha kubadilisha mwelekeo kuelekea Kaskazini Mashariki kwa kilomita 21.3 hadi Kituo cha Upimaji ZAE7, kisha kugeukia Mashariki kwa kilomita 46.16 kupitia vituo vya upimaji VP 716, VP 748, VP 720, hadi mahali pa kuanzia."

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)*

NEMBO YA HALMASHAURI YA MJI RUFIJI

Dodoma,
20 Disemba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*